Jarida la DCEA
TOLEO LA PILI JANUARI, 2023
ISSN NO. 978 - 9912 - 9896 - 1 - 0

# DAWA ZA KULEVYA

Kataa Dawa za Kulevya, Timiza Malengo Yako

## Wanasiasa, Viongozi wa Dini tumieni majukwaa yenu kupinga dawa za kulevya

HALIUZWI



Waziri Mkuu Wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) na Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Kudhibiti Dawa za Kulevya.

Kilo 877.217 za dawa za kulevya zakamatwa Dar na Arusha Uk.4

Polisi aliyefutwa kazi na kunusurika kifo kwa utumiaji dawa za kulevya ageuka nuru kwa waraibu Uk.8&9

Ijue Dawa ya Methadone katika kutibu uraibu wa dawa za kulevya Uk.12&13



## Yaliyomo


Wanasiasa, Viongozi wa Dini tumieni majukwaa yenu kupinga dawa za kulevya - Waziri Mkuu Majaliwa >>>



Uk.2

Siku ya Kitaifa ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani 2022 >>> Uk.3

Tutambue Mchango wa Wadau katika Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya >>>



Uk.6&7








Matukio Pichani >>> Uk.10&11

Ijue Dawa ya Methadone katika kutibu uraibu wa dawa za kulevya >>>



Uk.12&13

Waraibu wanufaika na Wiki ya Utumishi wa Umma >>>



Uk.20

Katuni >>> Uk.22

Tahariri

# *Mbinu Usafirishaji wa dawa za kulevya wakati wa Janga la UVIKO 19*



*UGONJWA wa Virusi vya Korona (UVIKO 19) umeleta mabadiliko katika mbinu za usafirishaji na mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Katika kipindi cha UVIKO 19, nchi nyingi zilifunga mipaka yake na mashirika mengi ya usafirishaji duniani yalisimamisha vyombo vya usafiri. Baadhi ya njia za usafirishaji kama vile kusafirisha shehena kubwa kwa kutumia meli, ndege binafsi, ndege zisizo na rubani, vifurushi pamoja na uuzaji wa dawa za kulevya kwa njia ya mtandao uliongezeka. Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Duniani ya Mwaka 2021 inaeleza kuwa, mauzo ya dawa za kulevya kwa njia ya mtandao (Dark web) yaliongezeka kutoka dola za kimarekani millioni 80 hadi dola millioni 315 kwa mwaka.*

*Biashara ya dawa za kulevya kwa njia ya mtandao ni hatari, kwani vijana wengi wanatumia mitandao ya kijamii hivyo kuwa na uwezekano wa kuyaona masoko ya dawa za kulevya mtandaoni. Wanunuzi wa dawa za kulevya kwa njia ya mtandao, hulipa pesa kwa njia ya mtandao na kupelekewa dawa hizo kwa njia ya vifurushi kupitia kwa wasafirishaji mbalimbali wa vifurushi kutumia majina ya bidhaa zingine ambazo ni halali.*

*Katika kipindi cha UVIKO 19, nchi yetu pia, ilishuhudia ukamataji wa kiasi kikubwa cha dawa za kulevya zilizoingizwa nchini kwa njia ya bahari. Mwezi Aprili, 2020 zilikamatwa kilo 268.5 za heroin eneo la Mbezi Kibanda cha Mkaa mkoani Dar es Salaam. Aidha, mwezi Aprili, 2022 zilikamatwa jumla ya Kilo 859.36 za dawa za kulevya zikijumuisha kilo 504.36 za heroin na kilo 355 za methamphetamine eneo la Kilwa Masoko mkoani Lindi. Pia, katika kipindi hicho, kilo 775 za dawa za kulevya aina ya mirungi zilikamatwa zikiwa zinasafirishwa kama vifurushi kwenda nchi za Ulaya na Marekani kwa majina ya bandia ya mlonge na kahawa.*

*Kutokana na mabadiliko katika mbinu za usafirishaji wa dawa za kulevya, Mamlaka inashirikiana na makampuni ya usafirishaji wa vifurushi ikiwemo Shirika la Posta, Vyombo vya Ulinzi na Usalama na wadau wengine katika mapambano ili kukabiliana na mbinu mpya za usafirishaji na uuzaji wa dawa za kulevya.*



*Gerald Musabila Kusaya*
***Kamishna Jenerali***

*Picha ya Jarida*



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,*
Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)

**Jarida hili limeandaliwa na**
Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

**BODI YA WAHARIRI**

**Mwenyekiti**
*Gerald Musabila Kusaya*
***Kamishna Jenerali***

**Katibu**
*Florence Khambi*
***Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano***

**Wajumbe**
*Dkt. Peter P. Mfisi*
*Salmin K. Shelimoh*
*Moza K. Makumbuli*
*Ziliwa P. Machibya*
*Christina G. Rweshabura*
*Upendo K. Chenya*
*Daniel M. Kasokola*
*Bushiri H. Matenda*
*Lilian B. Matho*

**SHUKRANI**

*Godfrey Nnko*
***Mwandishi wa Habari***

*Veronica Mrema*
***Mwandishi wa Habari***

*Haji Abeid*
***Msanifu na Mchora katuni***

Maoni ya Mhariri

# *Matumizi na Biashara ya dawa za kulevya ni changamoto kwa ustawi wa jamii*



DAWA za kulevya ni tishio duniani na ni tatizo linalovuka mipaka. Hivyo, tunahitaji ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika kukabiliana nalo.

Aidha, tatizo la dawa za kulevya hapa nchini bado ni kubwa. Takwimu zinaonesha kuwa mwaka 2014 kulikuwa na watumiaji kati ya 250,000 hadi 500,000. Wengi wa watumiaji hao walikuwa ni vijana. Hadi kufikia mwezi Desemba 2021, waraibu wa dawa mbalimbali za kulevya pamoja na vilevi vingine wapatao 905,902 walijitokeza kupata tiba katika hospitali za wilaya na mikoa nchini.

Dawa za kulevya hutumiwa na makundi mbalimbali ya kijamii hasa vijana. Bangi ni dawa ya kulevya inayotumiwa zaidi ikifuatiwa na heroin, mirungi na cocaine hapa nchini. Dawa nyingine zinazotumika ni dawa tiba zenye asili ya kulevya. Aidha, katika siku za karibuni kumekuwepo na matumizi ya ugoro na viyeyushi mfano gundi na petroli katika miji mikubwa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Mbeya, Arusha na Tanga.

Kwa kuwa watumiaji wengi wa dawa za kulevya ni vijana ambao ni nguvu kazi, matumizi ya dawa hizi huathiri maendeleo ya Taifa. Kwa sababu hiyo, nchi yetu imeendelea kukabiliana na tatizo la matumizi na biashara ya dawa za kulevya ili kuwalinda watanzania na athari zitokanazo na dawa hizo.

Kulingana na takwimu za Wizara ya Afya, maambukizi ya virusi vya UKIMWI (VVU) na magonjwa kama vile kifua kikuu, homa ya ini aina B na C yapo kwa kiasi kikubwa kwa waraibu wa dawa za kulevya ikilinganishwa na maambukizi ya VVU na magonjwa hayo kwenye jamii.

Hadi kufikia Disemba 2021, waraibu 967 kati ya 11,675 waliokuwa wamesajiliwa kupata huduma ya tiba kwenye vituo vya tiba saidizi kwa waraibu wa dawa za kulevya (MAT), walikutwa na maambukizi ya VVU ambayo ni asilimia 8.3 ikilinganishwa na asilimia 4.5 kwenye jamii. Aidha, waraibu 192 sawa na asilimia 3.33 walikuwa na maambukizi ya kifua kikuu ikilinganishwa na asilimia 0.13 katika jamii. Pia, waraibu 213 sawa na asilimia 3.7 walikuwa na maambukizi ya homa ya ini aina B. Waraibu 409 sawa na asilimia 7.1 walikutwa na maambukizi ya homa ya ini aina C ambapo maambukizi hayo kwenye jamii ni chini ya asilimia 2.

Aidha, matumizi ya dawa za kulevya husababisha uvunjifu wa amani katika jamii ikiwemo wizi, ukahaba, utapeli na unyang'anyi. Pia, matumizi ya dawa hizi huvuruga mahusiano kwenye familia, watoto kukosa malezi bora na kukimbilia mitaani na hivyo kusababisha watoto kukosa haki zao za msingi ikiwemo elimu.

Mara nyingi biashara ya dawa za kulevya husababisha uhalifu ikiwemo utakatishaji fedha, ugaidi, usafirishaji wa binadamu na ufadhili wa silaha za maangamizi.

Kama ilivyoelezwa hapo awali, bangi hutumiwa kwa wingi zaidi kuliko aina nyingine ya dawa za kulevya hapa nchini na kusababisha athari kwa watumiaji ikiwemo magonjwa ya akili kama vile sonona na psychosis. Pamoja na athari hizo, baadhi ya wanajamii wamekuwa na dhana potofu ya kutaka kuhalalisha kilimo na matumizi ya bangi. Hata hivyo, matumizi ya bangi ni kosa la jinai na imeharamishwa na Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Namba 5 ya Mwaka 2015.

Hata mataifa ambayo yamehalalisha matumizi ya bangi yanakutana na changamoto mbalimbali ikiwemo udhibiti wake. "Je? mzazi anaweza kuzungumza kuhalalishwa au matumizi ya kwa bangi kwa watoto nyumbani kwako". Kila mtu anawajibu wa kuunga mkono jitihada za Serikali za kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya.

*Florence Khambi*
***Mhariri***



WAZIRI Mkuu Wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akihutubia katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kitaifa ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya yaliyofanyika tarehe 2 Julai, 2022 katika viwanja vya Mnazimmoja jijini Dar es Salaam.

# Wanasiasa, Viongozi wa Dini tumieni majukwaa yenu kupinga dawa za kulevya - Waziri Mkuu Majaliwa

**Na. MWANDISHI Wetu**

WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) amewasisitiza viongozi wa vyama vya siasa na viongozi wa dini nchini kutumia majukwaa yao kukemea matumizi na biashara ya dawa za kulevya.

Ameyasema hayo tarehe 2 Julai 2022 akiwa mgeni rasmi, katika kilele cha Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani katika viwanja vya Mnazimmoja jijini Dar es Salaam yaliyokuwa na kauli mbiu **"Tukabiliane na Changamoto za Dawa za Kulevya kwa Ustawi wa Jamii"**

Mhe. Majaliwa aliwataka wanasiasa kuunga mkono juhudi za Serikali katika kupambana na dawa za kulevya kwa kukemea biashara ya dawa hizo wanapokuwa kwenye shughuli zao za kisiasa. Alisema, "Tumieni vikao vyenu vya ngazi mbalimbali vya ndani na nje pamoja na mikutano mnayoifanya kukemea biashara hii ya dawa za kulevya, mkemee matumizi ya dawa za kulevya, mkemee pia uzalishaji wa dawa za kulevya".

Aidha, aliwaomba viongozi wa dini wanapotoa mafundisho yao ya kiroho kutumia mwanya huo kukemea tatizo la dawa za kulevya. "Mnalo jukumu kubwa sana kwa jamii yetu ambalo mwenyezi Mungu amewapa la kutoa mafundisho ya kiroho. Wakati mkitekeleza jukumu hilo la kukemea dhambi na uovu wekeni pia msisitizo wa kukemea matumizi ya dawa za kulevya. Tunawategemea sana viongozi wa dini kwani mmefanya kazi kubwa na Serikali katika kufikisha ujumbe kwa jamii. Hivyo, tunaamini hii itakuwa moja ya ajenda ya kila muda wa sala pale kiongozi wa dini anapotoa mawaidha" alisema Waziri Mkuu Majaliwa.

> "Mnalo jukumu kubwa sana kwa jamii yetu ambalo mwenyezi Mungu amewapa la kutoa mafundisho ya kiroho. Wakati mkitekeleza jukumu hilo la kukemea dhambi na uovu wekeni pia msisitizo wa kukemea matumizi ya dawa za kulevya."

Kwa upande wa Wanahabari Waziri Mkuu aliwataka kutumia vyombo vyao kukemea kwa nguvu zote matumizi na biashara ya dawa za kulevya ikiwa ni pamoja na kutoa habari kuhusu huduma zinazotolewa kwa wathirika wa dawa hizo ili wale walioathirika waende kupata huduma.

Pia, ametoa wito kwa wasanii wote Nchini kutumia sanaa zao kukemea, kuelimisha na kuiongoza jamii kwenye mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Majaliwa aliwakumbusha wazazi na walezi kuendelea kuwalea watoto katika misingi na maadili ili kuwaepusha na vitendo viovu ikiwemo matumizi na biashara ya dawa za kulevya. "Turejee kwenye asili yetu ambapo jamii nzima ilihusika katika malezi ya watoto ikishirikiana katika kukemea uovu. Hivyo kila mmoja kwa nafasi yake ajione yeye ni mzazi na anawajibika kumlea mtoto yoyote wa kitanzania bila kujali kama mtoto huyo ni wake au la!" alisema Mhe. Majaliwa.

Vilevile, alisema mapambano dhidi ya dawa za kulevya yanahitaji ushiriki wa kila mmoja wetu. Hivyo, wananchi wote wenye taarifa za wafanyabiashara wa dawa za kulevya watoe taarifa kwa vyombo vya usalama ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa mapema na kwa haraka zaidi.

Maadhimisho

# Siku ya Kitaifa ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani 2022

**Na MWANDISHI Wetu**

MATUMIZI na biashara ya dawa za kulevya ni moja ya tishio kubwa kwa afya na jamii kwa ujumla ambalo ulimwengu unapambana nalo na linahitaji kupunguzwa kama si kuondolewa kabisa katika jamii. Kila mwaka Siku ya Kitaifa ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani hufanyika tarehe 26 Juni. Lengo kuu ni kuimbusha jamii juu ya madhara yatokanayo na dawa za kulevya ili iweze kushiriki kikamilifu katika udhibiti wa dawa hizo.

Tatizo la dawa za kulevya lilianza kutambulika kuwa ni changamoto kubwa ya kidunia mwanzoni mwa Karne ya 20. Kongamano la kwanza la kidunia kuzungumzia tatizo la dawa za kulevya lilifanyika katika mji wa Shanghai nchini China ambapo mwaka 1946 Umoja wa Mataifa uliunda Tume ya Dawa za Kulevya Duniani - Commission on Narcotic Drug (CND) ili kusimamia mikataba ya kimataifa ya udhibiti wa dawa za kulevya.

Mkutano wa CND uliofanyika mwezi Disemba mwaka 1987 uliazimia kuwa kila tarehe 26 ya mwezi Juni ya kila mwaka itumike kuadhimisha Siku ya Kitaifa ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani (The International Day Against Drug Abuse and Illicit Trafficking). Siku hii inalenga kuimarisha juhudi na ushirikiano wa kimataifa katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya ili kufikia lengo la kuwa na jamii ya kimataifa isiyo tumia wala kufanya biashara ya dawa za kulevya.

Tanzania kama mwanachama wa Umoja wa Mataifa ilianza kuadhimisha Siku ya Kitaifa ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani mwaka 1999. Maadhimishio haya huwashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo Taasisi za Serikali, Asasi za Kiraia, waraibu wa dawa za kulevya na jamii kwa ujumla. Maadhimisho hayo yameshafanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Dodoma, Iringa, Mbeya, Tanga pamoja na Pwani.

Tangu kuanzishwa kwa Mamlaka mwaka 2017, kumekuwepo na mafanikio katika udhibiti wa dawa za kulevya ambapo ukamataji wa wafanyabiashra wa dawa za kulevya umedhoofisha mitandao ya wafanyabiashara hao. Aidha, Mamlaka imeteketeza dawa za kulevya pamoja na kudhibiti matumizi na athari zitokanazo na matumizi ya dawa hizo.

Kwa mwaka 2022 Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani yalifanyika katika viwanja vya Mnazimmoja jijini Dar es Salaam. Kilele cha Maadhimisho hayo kilikuwa tarehe 2 Julai ambapo mgeni rasmi alikuwa Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wananchi walipata wasaa wa kutembelea mabanda ya maonesho na kupatiwa huduma mbalimbali ikiwemo elimu juu ya dawa za kulevya kwa njia ya maelezo, picha na machapisho.

Aidha, maandamano yaliyoongozwa na bendi ya polisi (brass band) yalihusisha wanafunzi, dereva bodaboda na wadau wengine waliobeba mabango yenye jumbe mbalimbali kuhusu dawa za kulevya. Pia, vikundi vya Sanaa viliburudisha na kuhamasisha Umma kushiriki katika udhibiti wa dawa za kulevya kupitia kazi zao.

Katika Maadhimisho hayo, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Mwongozo wa Utoaji Elimu kuhusu Tatizo la Dawa za Kulevya Nchini utakaotumika kuwasilisha elimu sahihi juu ya udhibiti wa dawa za kulevya kwa makundi mbalimbali. Kupita mwongozo huo, elimu husika itaifikia sehemu kubwa ya jamii na hatimaye kuongeza nguvu ya mapambano dhidi ya tatizo hilo.

Aidha, mgeni rasmi alizindua Riwaya ya Punje ya Tumaini inayohusu mapambano dhidi ya dawa za kulevya inayolenga kuonesha madhara ya moja kwa moja, kuwawajibisha na kuwafikisha mbele ya sheria wahusika na biashara haramu ya dawa za kulevya. Pia alitoa zawadi kwa waandishi wa habari watatu walioshinda shindano la uandishi bora wa walioandika taarifa za dawa kwa umahiri. Vilevile alitoa vyeti kwa wadau mbalimbali wanaojihusisha na mapambano ya dawa za kulevya Nchini.

Akizungumza katika kilele cha maadhimisho hayo, Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Gerald Musabila Kusaya alisema kuwa, tangu kuanzishwa kwa Mamlaka mwaka 2017, kumekuwepo na mafanikio katika udhibiti wa dawa za kulevya ambapo ukamataji wa wafanyabiashra wa dawa za kulevya umedhoofisha mitandao ya wafanyabiashara hao. Aidha, Mamlaka imeteketeza dawa za kulevya pamoja na kudhibiti matumizi na athari zitokanazo na matumizi ya dawa hizo.

Kamishna Jenerali, alimshukuru Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali anayoiongoza kwa kuunga mkono jitihada za udhibiti wa Dawa za Kulevya ikiwemo kukubali kusaini marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya mwaka 2021 pamoja na kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

# Kilo 877.217 za dawa za kulevya zakamatwa Dar na Arusha




*DAWA za Kulevya aina ya heroin zilizokamatwa mwezi Mei, 2022 jijini Dar es Salaam.*

**Na. MWANDISHI Wetu**

UKAMATAJI wa Dawa za Kulevya ni jukumu la msingi linalofanywa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kama nguzo muhimu katika kupunguza uingizaji, uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya Nchini. Jukumu hili hutekelezwa kupitia operesheni mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka kwa kushirikiana na vyombo vyingine vya Ulinzi na Usalama ndani na nje ya nchi.

Katika kipindi cha mwezi Mei 2022, Mamlaka ilikamata jumla ya kilo 877. 217 za dawa za kulevya zikihusisha Kilo 174.77 za heroin zilizokamatwa katika eneo la Tabata relini wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam zikimhusisha mtuhumiwa mmoja na kilo 703.105 za bangi zilizokamatwa mkoani Arusha zikiwahusisha watuhumiwa wanne. Watuhumiwa wote wamefikishwa mahakamani.






*SHAMBA la bangi likiteketezwa.*

> Katika kipindi cha mwezi Mei 2022, Mamlaka ilikamata jumla ya kilo 877. 217 za dawa za kulevya zikihusisha Kilo 174.77 za heroin zilizokamatwa katika eneo la Tabata relini wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam

Kwa upande wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya, Mamlaka inaendelea kufanya kaguzi za kufuatilia watu wanaokiuka taratibu za uingizaji na usambazaji wa kemikali bashirifu na dawa hizo ili kuzuia uchepushwaji.

Mafanikio haya yametokana na ushirikiano mkubwa ambao Mamlaka inaupata kutoka kwa wananchi kwa kutoa taarifa zilizosaidia kukamatwa kwa kiasi hiki cha dawa za kulevya, ambacho endapo kingeingia mitaani kingeharibu kwa kiasi kikubwa nguvu kazi ya Taifa. Mamlaka ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya inaendelea kutoa wito kwa wananchi kushiriki kikamilifu kupiga vita matumizi na biashara ya dawa za kulevya nchini.

# Kemikali bashirifu na dawa za kulevya

**Na. MWANDISHI Wetu**

KEMIKALI bashirifu ni Kemikali zinazotumika katika sekta mbalimbali za uzalishaji kama vile kilimo, migodi, maabara, kutengeneza dawa za binadamu na wanyama na kwenye sekta ya maji. Kemikali hizi zikichepushwa zinaweza kutumika katika mchakato wa kutengeneza dawa za kulevya. Kwa sababu hiyo, biashara na matumizi yake yanahitaji udhibiti madhubuti ili kuzuia zisitumike kutengeneza dawa za kulevya.

Udhibiti na usimamizi wa kemikali za majumbani na viwandani hufanywa chini ya Sheria ya Udhibiti na Usimamizi wa Kemikali za Viwandani na Majumbani [Sura 182] inayosimamiwa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Sheria hii imeainisha taratibu za udhibiti kuanzia uzalishaji hadi uteketezaji wa kemikali hizo. Taratibu zilizoainishwa ni pamoja na usajili, ukaguzi, na utoaji vibali vya kuingiza na kusafirisha kemikali.

Sheria nyingine inayodhibiti kemikali ni Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba [Sura 219] chini ya Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba. Sheria hii inadhibiti baadhi ya kemikali bashirifu zinazotumika kwenye uzalishaji wa dawa za binadamu. Udhibiti chini ya Sheria hiyo unafanyika kupitia usajili, kufanya ukaguzi na kutoa vibali vya kuingiza nchini kemikali hizo.

Aidha, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Namba 5 ya Mwaka 2015 [Sura 95] inakataza uchepushaji wa kemikali bashirifu kutumika kutengeneza dawa za kulevya;

Baadhi ya dawa za kulevya zinazotengenezwa kutokana na kemikali bashirifu ni pamoja na heroin, cocaine, methamphetamine, mandrax, amphetamine, na methadone.



*cocaine*



*heroin*



*mandrax*

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya inashirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo mamlaka za udhibiti na sekta binafsi kuzuia uchepushaji wa kemikali bashirifu kutumika kutengeneza dawa za kulevya. Miongoni mwa mamlaka za udhibiti ni pamoja na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA).

**Zifuatazo ni baadhi ya kemikali bashirifu zilizo chini ya udhibiti wa kitaifa na kimataifa**

| Acetic acid | Anthranilic acid |
|---|---|
| acetic anhydride | Chloroform |
| Acetone | Ephedrine |
| n-acetylanthranilic acid | Ergometrine |
| Acetyl chloride | Ethyl ether |
| Ethylidene diacetate | Ergotamine |
| Hydrochloric acid | 1-phenyl-2-propanone |
| Isosafrole | Phosphorous pentachloride |
| Lysergic acid | Phosphorous trichloride |
| 3,4-methylenedioxyphenyl-2-propanone | Piperidine |
| Methyl ethyl ketone | Potassium permanganate |
| Phenylacetic acid | 1-phenyl-2-propanone |
| Pseudoephedrine | Piperonal |
| Safrole | Thionyl chloride |
| Sulfuric acid | Toluene |

(pamoja na chumvi zitokanazo na kemikali hizo isipokuwa sulphuric acid na hydrochloric acid)



*Pseudoephedrine*



*Ephedrine*



*Acetic anhydride*

## Sheria inasemaje kuhusu kemikali bashirifu (makosa na adhabu)

Chini ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Sura ya 95 ya mwaka 2015 ni kosa kuchepusha kemikali bashirifu. Sheria hii imeanisha adhabu zifuatazo:

i. Kemikali bashirifu za hali ya kimiminika (liquid) zaidi ya lita 100 au zaidi ya kilogramu 100 ya kemikali bashirifu katika hali yabisi (solid) adhabu yake ni kifungo cha Maisha.

ii. Kemikali bashirifu katika hali ya kimiminika chini ya lita 100 au chini ya kilogramu 100 katika hali yabisi adhabu yake ni kifungo cha hadi miaka 30.

iii. Kuwezesha uchepushaji wa kemikali bashirifu ni kosa la jinai ambalo adhabu yake ni kifungo cha Maisha na faini isiyopungua shilingi bilioni moja.

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya inawahimiza wadau wote wanaojihusisha na kemikali bashirifu kuzingatia taratibu za kisheria.


# Tutambue Mchango wa Wadau katika Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya

Na. MWANDISHI Wetu

TATIZO la dawa za kulevya ni suala linalogusa nyanja mbalimbali hivyo kuhitaji nguvu ya pamoja katika kukabiliana nalo. Kutokana na hilo, wadau mbalimbali wamekuwa wakishiriki kwa namna moja au nyingine kuhakikisha wanakuwa sehemu ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Kwa kutambua umuhimu huo, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imewatunuku vyeti baadhi ya wadau wanaoshiriki katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Vyeti hivyo vilitolewa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) aliyekuwa mgeni rasmi katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kitaifa ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya kilichofanyika tarehe 02 mwezi Julai 2022, jijini Dar es Salaam.

## Mch. Richard Hananja

Ni mchungaji mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ambaye anatoa huduma za kiroho na kijamii kwa waraibu na familia zilizoathirika na tatizo la dawa za kulevya tangu mwaka 2013. Mchungaji Hananja ameanzisha asasi ya kiraia jijini Dar es Salaam inayoitwa Hananja Compassion Foundation yenye jukumu la kuwaunganisha waraibu na familia zao pamoja na kuwasaidia kuwapeleka katika vituo vya MAT na Nyumba za Upataji Nafuu ili kupata matibabu.



*Mch. Richard Hananja*

## SSP Andrew Gabriel Kantimbo

Ni Mkuu wa Upelelezi wa Polisi mkoa wa Mbeya aliyepata mafunzo ya upunguzaji madhara ya dawa za kulevya kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Dawa za Kulevya na Uharifu wa Kupangwa (UNODC). Amekuwa msaada katika kusaidia mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya katika mkoa huo kwa kuhakikisha waraibu wanaokabiliwa na makosa ya kihalifu waliopo mahabusu au kizuizini wanafikia Huduma za Methadone wakati wakisubiri hatma ya kesi zao. Pia amekuwa akielimisha askari juu ya tatizo la dawa za kulevya na umuhimu wa matibabu kwa waraibu.

## Changamoto ni Matumaini Sober House

Ni nyumba ya upataji nafuu (Sober house) iliyopo eneo la Boko jijini Dar es Salaam. Nyumba hii ilianza kufanya kazi mwaka 2009 na inatoa huduma bila malipo kwa vijana walioathiriwa na matumizi ya dawa za kulevya. Aidha, inauwezo wa kutoa huduma kwa waraibu 48 kwa wakati mmoja. Pia waraibu hao hupatiwa ujuzi wa fani mbalimbali ili kuwawezesha kujikimu kimaisha baada ya kukamilisha matibabu yao na kurejea katika familia zao.

## Said Bandawe

Ni katibu mtendaji wa Asasi ya Kiraia ya Gift of Hope Foundation ya jijini Tanga. Bandawe ni mraibu wa dawa za kulevya aliyepata nafuu tangu mwaka 2014. Tangu wakati huo amekuwa akishiriki kutoa elimu kwa jamii juu ya madhara ya dawa za kulevya pamoja na kuibua waraibu wa dawa za kulevya na kuwapeleka katika huduma za MAT na nyumba za Upataji Nafuu. Asasi yake imekuwa ikihamasisha upimaji wa magonjwa ya kuambukiza kwa waraibu pamoja na kuwapa mafunzo ya stadi za maisha ili kuwawezesha kiuchumi.

## Grace Albert Mbawala

Ni mraibu aliyepata nafuu tangu mwaka 2015. Amefanya kazi ya kusaidia kuhamasisha wanawake walioathirika na dawa za kulevya kujiunga na matibabu ya upataji nafuu katika vituo vya MAT kwa kushirikiana asasi ya kiraia ya MDM hadi mwaka 2019. Kwa sasa Grace anafanya kazi na asasi ya MKIKUTE iliyofanya shughuli zake jijini Dar es Salaam kama muelimishaji rika ngazi ya jamii.

## Elizabeth Mramba

Ni mwandishi wa riwaya, mshairi na mwandishi wa habari katika Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC). Ameandika riwaya ya "Punje ya Tumaini" inahusu mapambano dhidi ya dawa za kulevya ikilenga kuwawajibisha na kuwafikisha mbele ya sheria wanaohusika na biashara haramu ya dawa za kulevya. Riwaya hii pia imejikita katika kuonesha madhara ya moja kwa moja yanayowapata vijana pale wanapojiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya ambayo ni pamoja na kukatisha masomo na kupoteza mwelekeo wa maisha. Aidha, riwaya hiyo inaonesha namna waraibu wa dawa za kulevya wanavyoweza kupata tiba katika vituo vya afya au kwenye nyumba za upataji nafuu na kupata nafuu. Pamoja na mapambano dhidi ya dawa za kulevya riwaya hii ina maudhui ya kuwasadia vijana kujitambua na kujiepusha na vishawishi, suala la uzalendo pamoja na madhara ya ukatili wa kinjinsia.

*(Picha zaidi za wadau zipo ukurasa wa 7.)*

# Baadhi ya wadau wakitunukiwa vyeti kutambua mchango wao katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya



*WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akimtunukia cheti Mkurugenzi wa asasi ya kiraia ya Hananja Compassion Foundation Mch. Richard Hananja.*



*WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akimtunukia cheti Mkuu wa Upelelezi wa Polisi mkoa wa Mbeya SSP Andrew Gabriel Kantimbo.*



*WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akimtunukia cheti Antony Fredrick, mkurugenzi wa Nyumba ya Upataji Nafuu ya Changamoto ni Matumaini iliyopo jijini Dar es Salaam.*



*WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akimtunukia cheti Katibu Mtendaji wa asasi ya kiraia ya Gift of Hope Foundation ya jijini Tanga ndugu Said Bandawe.*



*WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akimtunukia cheti Grace Mbawala muelimishaji rika kutoka asasi ya MKIKUTE.*



*WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akimtunukia cheti Elizabeth Mramba Mwandishi wa Riwaya, Mshairi na Mwandishi wa Habari wa Shirika la Utangazaji Tanzania – TBC.*

# Polisi aliyefutwa kazi na kunusurika kifo kwa utumiaji dawa za kulevya ageuka nuru kwa waraibu

Na MWANDISHI Wetu

NAITWA Twaha Amani, mzaliwa wa Pasua mkoani Kilimanjaro. Nilianza kuvuta bangi nikiwa kidato cha pili na mpaka nilipohitimu kidato cha sita nilijikuta ni mtumwa wa matumizi ya bangi. Wakati nasubiri matokeo, nilianza kazi ya kunyoa na nilinunua mashine ya kunyolea nikawa naikodisha kwa kinyozi jirani, jioni nikifunga saluni ninapitia kwake kuchukua fedha zangu. Siku moja nilipoenda kuchukua fedha, nilimkuta jamaa anavuta "unga" akanipa nijaribu kuvuta.

Nilipojaribu nikajisikia mtu wa tofauti. Kesho yake akanipa tena kidogo na aliniambia hiyo ni heroin, hivyo nimchangie shilingi 600 ili tuongezee. Safari yangu ya "unga" ilianzia hapo 2006. Wakati huo matokeo ya chuo yalikuwa yametoka na nilipata ufaulu wa daraja la tatu. Nikiwa nasubiri kuniunga na chuo, nilipata ajira ya muda ya kusoma mita za umeme, kasi ya matumizi ya heroin yaliongezeka kutokana na kipato nilichokuwa nakipata kutokana na ajira hiyo.

Mwaka 2007 nilijiunga na Chuo cha Polisi Moshi. Nikiwa mafunzoni nilikuwa nabanwa na ratiba hivyo nilitumia "unga" siku za mapumziko tu. Baada ya kuhitimu niliripoti Tabora kwenye kituo changu cha kazi. Siku moja nikiwa zamu, kijana aliyekuwa ananiuzia bangi alikamatwa na mirungi na kuletwa kituoni. Tukiwa kwenye kupiga stori nikamuuliza wapi wanauza "unga" akanipeleka, waliniuzia japo walijiuliza kwamba na huyu askari ananunua au anatuchora? Baada ya hapo nilimsaidia yule kijana kupoteza vithibiti vyake (mirungi) na akaachiwa huru.

Kasi ya uvutaji wa heroin iliongezeka na mambo yakazidi kuwa mabaya. Hata hivyo, "unga" ulikuwa haupatikani kirahisi Tabora hivyo, tulilazimika kujichangisha fedha na kumpa 'mzungu' ambaye alituagizia jijini Dar es Salaam na kutumwa Tabora kwa treni. Kutokana na matumizi ya "unga" kukithiri mwaka 2009 nilifukuzwa kazi ikanibidi nirudi Moshi. Nilikaa mtaani baadaye nikaanza kujidunda sindano kutokana na stress za kufukuzwa kazi huku nikiiba vitu mtaani na

**MUHTASARI**

**1983**
Kuzaliwa

**2006**
Kuanza Unga

**2007**
Kujiunga Chuo cha Polisi Moshi

**2009**
Kufukuzwa Upolisi

**2009**
Kujiunga na Chuo cha Ualimu Marangu

**2010**
Kusimamishwa chuo baada ya kumjeruhi mwenzangu aliyekuwa ananidai shilingi elfu kumi

**2011**
Kurudishwa chuoni

**2012**
Ajira ualimu

**2020**
Kupelekwa Sober House

**2021**
Kufungua Sober House binafsi

kukitokea kazi za kupandisha wazungu Mlima Kilimanjaro nafanya. Mama yangu alikuwa anafahamiana na Afisa Elimu wa Mkoa, hivyo akamuomba amsaidie nipate kazi.

Mwaka huo huo nilichaguliwa kujiunga na Chuo cha Ualimu Marangu. Nikiwa Chuoni nilianza kuvuta heroin na kuiba usiku. Nikiwa mwaka wa pili nilisimamishwa chuo baada ya kumjeruhi mwenzangu aliyekuwa ananidai shilingi elfu kumi. Mwaka 2011 nilirudishwa chuoni ikabidi niache kuvuta ili nizingatie masomo ambapo nilimaliza mtihani na tukarejea nyumbani kusubiri matokeo ya diploma ya ualimu wa sekondari.

Matokeo yalitoka nikiwa nimefaulu vizuri na nikapangiwa kwenda kufundisha Shule ya Sekondari Kasororo huko Misungwi vijijini mkoani Mwanza. Mama yangu alinipatia pesa za kunisaidia nikiwa huko, na baada ya kufika kituoni tulipewa fedha za kujikimu, lakini nilitumia pesa zote kununua dawa za kulevya. Baada ya muda nikaanza kukopa na madeni yalipozidi nikaacha kazi na kukimbilia Mwanza mjini na kuendelea na vitendo vya wizi.

Siku moja nilikamatwa na kupelekwa kituo cha Polisi. Nikiwa hapo nikamuona askari niliyefahamiana naye Chuo cha Polisi Moshi. Nikamuelezea mkasa wangu wote, japo mwanzoni tulipokuwa tunakutana mtaani Mwanza nilikuwa namdanganya kwamba ninafundisha. Akawasiliana na ndugu zangu na kuwaeleza kwamba niko mahabusu.

Mahakama iliniachia huru kwa masharti ya kutoonekana tena mkoa wa Mwanza. Baada ya hapo nilisafirishwa mpaka nyumbani Mkoani Kilimanjaro ambapo nilifungiwa chumbani kwa muda wa miezi sita. Baada ya kutolewa nje, Anko wangu akawa ananipitia tunaenda kwenye mashamba yake ya mpunga huku akiangalia kama nimebadilika, lakini mimi nikaendelea kuvuta "unga" na baadaye nikamtoroka nikaingia mtaani.

Huko mtaani nilikutana na jamaa ambaye alikuwa

*Inaendelea Ukurasa wa 9*

Shuhuda

# Polisi aliyefutwa kazi, kunusurika kifo

*Inatoka Ukurasa wa 8*

ni mwizi akanishawishi nikakae nyumbani kwao. Nikakubali na tukawa tunaenda wote kwenye mizunguko ya wizi. Siku moja katika harakati za wizi tulivunja nyumba kadhaa watu wakatushtukia na kupiga kelele, tulikimbia ila walimkamata rafiki yangu wakampiga mpaka wakamuua.

Kutokana na tukio hilo, ilinibidi niende nyumbani moja kwa moja, nikakuta taarifa zimeshasambaa mtaani kwamba nilikuwa na huyo aliyeuawa usiku. Ndugu zangu wakawa wananishawishi nikimbilie Arusha, lakini Anko wangu akasema hata nikipelekwa huko watanikamata kwani ni karibu, bora nipelekwe jela. Wakanipakiza kwenye gari, njiani wakanunua mafuta ya petroli na kibiriti wakanipeleka mpaka Kituo cha Polisi, na kusingizia kwamba nilitaka kuchoma moto nyumba tunayoishi. Nilikaa mahabusu katika gereza la Karanga kwa muda wa miezi sita na baadaye niliachiwa huru na Mahakama.

Nikarudi nyumbani lakini nikaendelea kuvuta "unga". Wakati huo kuna watu kutoka Zanzibar walikuja Moshi kule Bomang'ombe, wakafungua Sober House, hivyo wakawa wanatafuta waathirika wa dawa za kulevya ili wajiunge na sober yao. Walifika nyumbani kwetu na kueleza faida za huduma hiyo na nilikubali kujiunga.

Baada ya siku tatu nilitoroka, nikaenda mpaka kazini kwa mama nikamdanganya kwamba wale jamaa ni matapeli. Nikiwa nyumbani hali ikawa mbaya zaidi ya mwanzo, nilipata mateso makubwa ikawa kama laana kabisa. Baada ya miezi mitatu ilibidi nirudi mwenyewe kule Sober kuomba msaada. Mwaka 2016 ukatokea ugomvi kati yangu na mwenye Sober hivyo akanifukuza ikanibidi nirudi nyumbani nikaanza tena kuvuta "unga".

Anko alinipa kazi ya kusimamia mashine ya kukoboa mpunga na kuuza mchele. Ikawa mchana niko kazini ila usiku naenda kuiba. Siku moja nilikamatwa na kupigwa sana. Mama alifanya jitihada nikarejeshwa Sober House ambako nilikaa kwa miaka mitatu nilipona na kurejea katika hali yangu ya kawaida. Nilipotaka kuondoka mmiliki wa nyumba hiyo alinitaka niendelee kukaa hapo kwa ahadi ya kuniajiri.





Nikaendelea kufanya kazi, nikiwa hapo Sober nilingia kwenye mahusiano na dada jirani na Mwaka 2019 tulibahatika kupata mtoto. Kutokana na majukumu kuongezeka, ikabidi niende Mwanza katika Halmashauri ya Misungwi kufuatilia ajira yangu ya ualimu niliyoajiriwa mwaka 2012 hata hivyo nafasi yangu haikuwepo tena. Hivyo, nilirejea na kuendelea na kazi kama Meneja wa Sober House hiyo.

Kutokana na uzoefu katika kuhudumia na kusimamia sober house hizi, nilipata shauku ya siku moja kufungua Sober House yangu. Mwaka 2021, katika eneo la Himo Mkoani Kilimanjaro nilifanikiwa kufungua sober na sasa ni Mkufunzi na Mkurugenzi wa Sober House iitwayo **Surrender for Freedom Teatment Center** yenye waraibu 27.

Ujumbe wangu wa vijana na jamii kwa ujumla ni kwamba, mimi nilianguka, sasa nimesimama tena nikiwa imara na niko mstari wa mbele kuhakikisha ninashirikiana na Serikali na jamii kupiga vita matumizi na biashara ya dawa za kuelvya. Vijana tuepuke na kuachana na makundi yasiyo na umuhimu kwetu, tufanye kazi kwa bidii na kujikita katika mambo ambayo yatatusaidia kuzifikia ndoto zetu.

Twaha ni kijana aliyewakilisha makundi ya vijana wanaopitia changamoto kadhaa kutokana na matumizi ya dawa za kulevya. Ushuhuda wake umeonesha sababu zinasababisha watu kujiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya ikiwemo kujihusisha na makundi hatarishi. Wazazi na walezi wana wajibu wa kufuatilia nyendo ya watoto wao na kuwaongoza katika njia zilizo sahihi.

*JUU: Twaha Amani wakati wa matumizi ya dawa za kulevya. CHINI: Baada ya kuacha.*

# Matukio Pichani




*WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akipata maelezo kuhusu kazi zinazofanywa na Mamlaka katika kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya kutoka kwa Ziliwa Machibya Kamishna Msaidizi na Sayansi Jinai.*



*WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Mu Majaliwa (Mb) akipata maelezo ku ya Kitaifa ya Siku ya Kupinga Matu*



*KAMISHNA Jenerali Gerald Musabila Kusaya (wa tatu kushoto) pamoja na wakuu wa vyombo vinavyohusika na mapambano dhidi ya dawa za kulevya wakiwa Johannesburg - Afrika Kusini katika kikao kilicholenga kujadili masuala yanayohusu mapambano dhidi ya dawa za kulevya baina ya nchi za Tanzania, Msumbiji na Afrika Kusini (Trilateral States).*






*BALOZI wa Uingereza Nchini Tanzania David Concar akimkabidhi Kamishna Jenerali nyaraka za magari yaliyotolewa na Ubalozi huo kwa Mamlaka kama sehemu ya kusaidia mapambano ya dawa za kulevya nchini.*



*SEHEMU ya uteketezaji wa hekari 21 za Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Monduli mkoni Arusha.*



: Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa
o kutoka banda la MDH kwenye kilele cha Maadhimisho
Matumizi na Biashara ya Dawa za Kulevya.



*MKURUGENZI Huduma za Kijamii wa Shirika HJFMRI Bi. Hijja Wazee akipokea toleo la kwanza la Jarida la dawa za kulevya kutoka kwa Daniel Kasokola Afisa Mawasiliano Mwandamizi wa Mamlaka.*



*WANAFUNZI wakifuatilia kwa umakini maelezo kuhusu tatizo la dawa za kulevya kutoka kwa Queen Komba Afisa Elimu wa Mamlaka.*



*MKUU wa mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Amosi Makalla na mgeni rasmi katika ufunguzi wa Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Kupinga Matumizi na Biashara ya Dawa za Kulevya kutoka kwa Afisa Sheria wa Mamlaka Bryson Ngidos.*



l za Mashamba ya bangi uliofanywa na
ia na Dawa za Kulevya katika Wilaya ya

*KAMISHNA wa Kinga na Tiba wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Dkt. Peter Mfisi akitoa mada kuhusu tatizo la dawa za kulevya katika kikao cha uhamasishaji wa mapambano dhidi ya dawa hizo mkoani Arusha.*



# Ijue Dawa ya Methadone katika kutibu uraibu wa dawa za kulevya

Na. MWANDISHI Wetu

## Methadone ni nini?

METHADONE ni dawa inayotumika kutibu utegemezi wa dawa za kulevya zenye asili ya afyuni ikiwemo heroin, Morphine na pethidine. Dawa hii hutolewa katika vituo vya kutoa tiba saidizi kwa waraibu wa dawa za kulevya (Medically Assisted Therapy-MAT) vilivyopo katika hospitali na vituo vya afya nchini.

Tanzania imekuwa nchi ya kwanza katika ukanda wa nchi za jangwa la sahara (Sub-Saharan African Countries) kutoa matibabu ya utegemezi wa dawa za kulevya kwa kutumia dawa ya Methadone baada ya kuanzisha kituo cha MAT katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili mwaka 2011.

## Je, ni nani anaweza pata dawa ya Methadone?

Mtu yeyote aliye na tatizo la uraibu au utegemezi wa dawa za kulevya wa dawa zenye asili ya afyuni kama vile Heroin na dawa zenye asili ya kulevya zinazotumika kutibu magonjwa mengine mfano wa Pethidine, Tramadol, Morphine na kadhalika. Methadone hutolewa chini ya uangalizi wa watoa huduma za afya kwa wagonjwa waliothibitishwa kuwa na uraibu wa dawa za kulevya tajwa baada ya kufanyiwa vipimo mbalimbali.

## Je, mraibu hutakiwa kupata tiba ya Methadone kwa muda gani?

Matibabu kwa kutumia dawa ya methadone huchukua sio chini ya miaka miwili (2) ambayo hutegemea mraibu ameathirika kwa kiwango gani, aina ya dawa na kiasi cha dawa aliyokuwa akitumia ikiwa ni pamoja na hali ya afya ya mraibu.




## Faida za Matibabu ya Methadone ni zipi?

Utoaji wa tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya kwa kutumia methadone umeonesha manufaa ya moja kwa moja kwa waraibu na jamii kwa ujumla.

Yafuatayo ni baadhi ya manufaa yanayotokana na huduma hiyo:-

i. Kuondoa utegemezi wa dawa za kulevya aina ya heroin na dawa tiba zenye asili ya kulevya na hatimaye kuwarejeshea nguvu waraibu na kuwawezesha kushiriki katika ujenzi wa Taifa.

ii. Methadone imechangia kupunguza hatari ya mtumiaji kuambukizwa magonjwa yatokanayo na utumiaji wa dawa za kulevya kama vile VVU, homa ya ini , kifua kikuu na magonjwa ya ngono pamoja na kuimarisha mfumo wa uzazi;

iii. Methadone hufanikisha kurejesha hali ya afya ya mtumiaji wa dawa za kulevya na kurudisha imani na faraja kwa jamii inayomzunguka;

iv. Utoaji wa dawa ya Methadone umechangia kupunguza kundi kubwa la wahalifu, kesi mahakamani, wafungwa magerezani uvunjaji wa amani na usalama katika jamii na Taifa;

v. Hupatikana bure katika vituo vyote vya MAT vilivyo katika hospitali za serikali;

vi. Ndugu na jamaa huusishwa katika utaratibu wa matibabu ya upaji nafuu ili kusaidia mahitaji kama chakula, nauli na malazi ambayo kufanikisha upataji nafuu;

vii. Methadone imekuwa chanzo kwa waraibu kupata matibabu ya mgonjwa mengine kama vile VVU, homa ya ini, na kifua kifuu ikiwa ni pamoja na kupata rufaa; pamoja na,

viii. Methadone imekuwa chanzo cha waraibu kupata mahitaji mengine ikiwemo ujuzi na stadi za maisha.

## Je, ni kweli Methadone huwa na athari za kiafya kwa watumiaji?

Methadone ni dawa salama kwa matibabu ya uraibu wa heroin na dawa nyingine zenye asili ya afyuni. Hata hivyo, imethibitika kuwa na maudhi madogo madogo yaliyovumilivu ambayo huonekana kama vile: kichefuchefu, kutapika, athari za muda za kupata choo, maumivu ya kichwa, kukauka kwa midomo, usingizi na kutokwa kwa jasho ambayo hutokea kwa baadhi ya wagonjwa wanapoanza matibabu na kuisha baada ya muda mwili unapozoea dawa hiyo.

## Angalizo:

Matumizi yasiyo sahihi ya Methadone huweza kusababisha kifo. Hivyo, dawa hii inatakiwa kutolewa chini ya uangalizi wa wataalam wa huduma za afya kwa viwango sahihi ili kupunguza vifo vinavyoweza kutokea kutokana na matumizi yasiyo sahihi kama vile kuzidisha dozi.

*Inaendelea Ukurasa wa 13*

# Dawa ya Methadone na faida zake



*KLINIKI ya Tiba Saidizi - MAT iliyopo katika hospitali ya Mount Meru Jijini Arusha.*

*Inatoka Ukurasa wa 12*

## Taratibu za upataji wa huduma za tiba kwa kutumia Methadone katika vituo vya MAT zikoje?

Serikali imekuwa ikitoa huduma za matibabu kwa waraibu wa dawa za kulevya kwa kushirikiana na asasi za kiraia zenye jukumu la kutafuta waraibu wa dawa za kulevya katika jamii, kuwaandaa waraibu hao kwa kuwapatia mafunzo kwa takribani wiki mbili kabla ya kujiunga na matibabu katika vituo vya MAT.

## Tiba ya Methadone inatolewa wapi?

Hadi kufikia Julai 2022 nchi ya Tanzania imefanikiwa kuwa na vituo 15 vinavyotoa tiba saidizi kwa waraibu wa dawa za kulevya kwa kutumia dawa ya Methadone ambavyo vimesajili jumla ya waraibu 13,094.

Tangu mwaka 2011, vituo vya MAT vimekuwa vikianzishwa kwenye mikoa yenye idadi kubwa ya watumiaji na waathirika wa matumizi ya dawa za kulevya. Vituo hivyo vipo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Tanga, Mwanza, Dodoma, Mbeya, Songwe na Pwani (Rejea jedwali chini).

## Vituo vya MAT vinavyotoa dawa ya Methadone nchini:

| S.Na | Jina la Kituo | Jina la Hospitali | Mkoa |
|---|---|---|---|
| 1. | MAT Muhimbili | Hospitali tya Taifa ya Muhimbili | Dar es Salaam |
| 2. | MAT Mwananyamala | Hospitali ya Mkoa ya Rufaa ya Mwananyamala | Dar es Salaam |
| 3. | MAT Temeke | Hospitali ya Mkoa ya Rufaa ya Temeke | Dar es Salaam |
| 4. | MAT-Mbeya | Hospitali ya Kanda ya Rufaa ya Mbeya | Mbeya |
| 5. | MAT-Mwanza | Hospitali ya Mkoa ya Rufaa ya Sekou Toure | Mwanza |
| 6. | MAT-Itega | Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe | Dodoma |
| 7. | MAT-Bagamoyo | Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo | Pwani |
| 8. | MAT-Tanga | Hospitali ya Mkoa ya Rufaa ya Bombo | Tanga |
| 9. | MAT-Tumbi | Hospitali ya Wilaya ya Tumbi-Kibaha | Pwani |
| 10. | MAT-Arusha | Hospitali ya Mkoa ya Rufaa ya Mount-Meru | Arusha |
| 11. | MAT-Tunduma | Kituo cha Afya Wilaya ya Tunduma | Songwe |
| 12. | MAT-Segerea | Kituo cha Afya cha Segerea | Dar es Salaam |
| 13. | MAT-Tegeta | Kituo cha Afya cha Tegeta | Dar es Salaam |
| 14. | MAT-Mbagala | Kituo cha Afya cha Round Table -Mbagala | Dar es Salaam |
| 15. | MAT-Kigamboni | Kituo cha Afya cha Vijibweni-Kigamboni | Dar es Salaam |

# Ijue bangi na madhara yake

Na. MWANDISHI Wetu

BANGI ni aina ya dawa ya kulevya inayotokana na mmea unaoitwa "Cannabis sativa" ambao hustawi kwa wingi hapa nchini na maeneo mengi duniani. Bangi huweza kuwa katika hali mbalimbali kama vile majani yaliyokaushwa, bangi iliyosindikwa (cannabis resin) ambayo hufahamika kama charas au hashish na hali ya mafuta. Aidha, baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakiweka bangi kwenye vyakula mbalimbali kama keki, biskuti na koni.

Mmea wa bangi unakadiriwa kuwa na kemikali zaidi ya 400. Hata hivyo, kemikali inayo leta madhara makubwa kwa binadamu ni THC (delta-9-tetrahydrocannabinol). Sehemu kubwa ya kemikali hii hupatikana katika majani na maua ya bangi na kiasi kidogo hupatikana katika shina na mizizi.



*Mafuta ya bangi.*

Inakadiriwa kuwa, kwa kawaida mmea wa bangi una kiwango cha kati ya asilimia 10 hadi 20 ya kemikali ya THC. Hata hivyo, baadhi ya waharifu wanatumia teknolojia kuzalisha bangi yenye kiwango kikubwa cha THC cha hadi asilimia 70. Kadri bangi inavyokuwa na kiwango kikubwa cha THC ndiyo inakuwa na madhara zaidi kwa matumizi ya binadamu.

Bangi iliyosindikwa huwa na kiasi kikubwa cha kemikali hiyo inayofikia asilimia 40 ikilinganishwa na bangi ya majani iliyokaushwa. Kiasi kikubwa cha bangi iliyosindikwa huzalishwa kwa kutumia maua na vikonyo vya bangi katika nchi za Morocco, Lebanoni na Afghanistan.





*BISKUTI zilizotengenezwa kwa bangi.*

Aidha, wahalifu wanaotengeneza bidhaa za vyakula za bangi kama vile biskuti, pipi na keki, huweka kiasi kikubwa cha THC hadi kufikia asilimia 70. Ulaji wa bidhaa hizo unaweza kusababisha madhara makubwa.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Duniani ya Mwaka 2022, bangi hutumika zaidi kuliko dawa nyingine za kulevya. Inakadiriwa kuwa Mwaka 2021 takribani watu milioni 209 duniani walitumia bangi.

## Madhara ya bangi yanategemeana na;

Kiasi cha uvutaji: Kadri inavyovutwa kwa wingi ndivyo inavyoleta madhara zaidi.

Kiwango cha THC katika bangi: Bangi yenye kiwango kikubwa cha THC ina madhara zaidi

Njia ya utumiaji: Wale wanaokula bidhaa za bangi hudhurika zaidi

Maumbile ya binadamu: Baadhi ya watu wanaweza kuhimili na wengine hudhurika zaidi

*Inaendelea Ukurasa wa 15*

Inatoka Ukurasa wa 14

## Madhara ya muda mfupi


- Kuchanganyikiwa
- Kupoteza kumbukumbu, umakini na usikivu
- Uwoga na hali ya wasiwasi
- Kushindwa kufanya maamuzi ya haraka
- Kuongezeka hali ya kushuku ***(paranoia)***
- Hisia za uongo ***(delusions)***
- Kuhisi vitu ambavyo havipo ***(hallucinations)***
- Kupata hisia mchanganyiko ***(mood disturbances)***
- Kushuka kwa presha

## Madhara ya muda mrefu


- Huathiri mfumo wa fahamu na kumfanya mtu kuona, kusikia au kuhisi vitu pasipo uhalisia ***(hallucinations)***
- Huamsha magonjwa ya akili kama vile; sonona, psychosis, kihoro, schizophrenia
- Kupoteza uwezo wa kufikiria na kufanya maamuzi sahihi



- Kupoteza kumbukumbu
- Hali ya wasiwasi na kushuku **(paranoia)**
- Husababisha mapigo ya moyo kwenda mbio na mishipa ya damu kutanuka pamoja nakushuka kwa presha



- Husababisha magonjwa ya mapafu ikiwemo kansa ya mapafu pamoja na kiarusi



- Kupoteza uwezo wa kufanya kazi kwa ukamilifu
- Husababisha utegemezi, kukosa mwamko wa maendeleo



- Ni chanzo cha dawa zingine za kulevya kama vile Heroin Kokein n.k.

## Madhara ya kilimo cha bangi

Mara nyingi, kilimo hufanyika katika maeneo yaliyojificha hasa kwenye misitu mikubwa na milimani, maeneo ambayo vyombo vya ulinzi na usalama haviwezi kufika kirahisi. Wakulima hawa wamekuwa wakikata misitu ya asili na kupanda bangi. Hivyo, hupunguza mvua, hukausha vyanzo vya maji, husababisha mmomonyoko wa ardhi, kutoweka kwa viumbe hai na kuharibu uoto wa asili.

## Uhalalishaji wa bangi

Mwaka 2020, kamisheni ya Kimataifa inayodhibiti dawa za kulevya (CND), ililegeza baadhi ya vipengele vya udhibiti wa bangi ili nchi nyingi ziweze kuruhusu kilimo cha bangi kwa ajili ya matumizi ya dawa na tafiti za kisayansi. Hata hivyo shirika hilo liliendelea kusisitiza kuwa bangi iendelee kuwa




Kilimo hicho lazima kifanyike kwenye kitalu nyumba **(Green House)** ili kuhakikisha kuwa hapatokei mchanganyiko **(cross pollination)** na bangi ya kienyeji.

dawa inayodhibitiwa duniani kwakuwa ikitumika kwa ajili ya kusitarehesha ina madhara makubwa.

Baadhi ya nchi zimeruhusu kilimo cha bangi kwa ajili ya matumizi ya kutengenezea dawa. Kemikali za kwenye bangi zinazoweza kutumika kutengenezea dawa ni tetrahydrocannabinol (THC) na cannabidiol (CBD). Kama ilivyoelezwa hapo awali, THC ni kemikali inayosababisha madhara kwa watumiaji wa bangi, ikiwemo uharibifu wa mfumo wa fahamu na utegemezi. Kutokana na hali hiyo, kemikali aina ya CBD ndiyo inayotakiwa zaidi kwenye utengenezaji wa dawa kwa kuwa haina kilevi na wala haileti utegemezi.

Kutokana na hali hiyo, bangi inayotumika kutengenezea dawa za tiba inatakiwa iwe na kiwango kikubwa cha CBD na kiwango kidogo sana cha THC (chini ya asilimia 0.3) ili watumiaji wa dawa hizo wasipate utegemezi (Addiction). Bangi inayolimwa hapa nchini haifai kabisa kutumika kutengenezea dawa za tiba kwa kuwa inakiwango kikubwa cha THC.



# Biashara ya dawa za kulevya ilivyoharibu maisha yangu

**Na MWANDISHI Wetu**

NAITWA Sarah Kilemike (36) ni mama wa watoto watatu niyeathiriwa na matumizi ya dawa za kulevya aina ya heroin. Niliingizwa kwenye biashara ya dawa za kulevya na ndugu zangu waliokuwa wanafanya biashara hiyo kwa lengo la kupata utajiri wa haraka. Walinifundisha jinsi ya kumeza kwa kutumia unga wa sembe waliufunga kwa mfano wa pipi.

Baada ya kufanikiwa darasa hilo, nilipata safari ya kwanza kwenda kufuata mzigo (dawa za kulevya) wa kaka yangu nje ya nchi. Nilirudi salama kupitia uwanja wa ndege wa Kilimanjaro na nikapata pesa nyingi.



Wakati wa safari ndefu nililazimika kunusa kitu kiitwacho "kata mavi" kwa lengo la kukata haja kubwa ili nifikishe mzigo salama. Binafsi sikujua kwamba "kata mavi" ni dawa za kulevya na kitendo hicho kingeathiri afya yangu siku za usoni.

Haikuwa kazi nyepesi kusafirisha dawa za kulevya hadi kwa mteja aliyeagiza mzigo huo, kwani kuna wakati unakumbwa na mfadhaiko wa kisaikolojia hasa ukihofia zinaweza kupasukia tumboni, maana unameza kitu ambacho hujui aliyefunga alifunga vizuri au la!

Baada ya muda nilianza kuuza kila nilichokipata kimoja baada ya kingine, isipokuwa nyumba ambayo naishi. Nilianza kutumia kidogo kidogo na baadaye nikawa mraibu kabisa. Sikuweza tena kusafirisha mzigo.

Nashukuru nilijiunga na tiba saidizi ya methadone katika hospital ya Mwananyamala mpaka sasa nimeachana na matumizi ya dawa za kulevya na ninaendelea vizuri. Huko mtaani kuna wanawake wengi wameathirika na dawa za kulevya lakini bado hawajitokezi kupata tiba. Naomba wasijifiche bali wajitokeze kupata tiba kwani methadone inasaidia na imerejesha matumaini yangu.

Naishukuru Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, nawashukuru wauguzi wote wanaosaidia kufanikisha tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya, nawashukuru MDH, naishukuru Serikali kwa kutoa huduma ya methadone bure, pia nawashukuru wanaharakati wote wanaopambana na dawa za kulevya.

Nitoe wito wa vijana wenzangu kuachana na matumizi ya dawa za kulevya kwani yanakatisha ndoto na kupoteza mwelekeo, unaweza kuanza kama starehe lakini baadaye inakuwa majuto. Hivyo nawashauri kutokujiingiza kabisa kwenye biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

Tuzo

# Watatu Wang'ara Tuzo za Uandishi Bora wa Habari za Dawa za Kulevya

**Na. MWANDISHI Wetu**

WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), amewatunukia tuzo ya umahiri wa uandishi bora wa habari zinazohusu dawa za kulevya washindi watatu kutoka vyombo vya habari vya mtandaoni (digital journalists). Mshindi wa kwanza ni Veronica Romwald Mrema kutoka Matukio na maisha blog aliyepata cheti na pesa taslimu shilingi 500,000 akifuatiwa na Abel Kilumbu kutoka Dar 24, alipata cheti na shilingi 450,000, huku John Laurent kutoka JMTZ Media akishika nafasi ya tatu na kupata cheti na shilingi 400,000.

Tuzo hizo zimetolewa katika kilele cha Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya yaliyofanyika tarehe 02 Julai, 2022 katika viwanja vya Mnazimmoja jijini Dar es Salaam.

Kabla ya utoaji wa tuzo hizo, Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Gerald Kusaya alisema, Mamlaka imetoa tuzo hizo kwa mara ya kwanza ili kutambua mchango wa wanahabari na kuongeza ari ya mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya.

Aidha, alisema, mwezi Februari, 2022 Mamlaka iliandaa shindano la kumtafuta mwandishi wa habari za kimtandao aliyeandaa habari bora juu ya tatizo la dawa za kulevya kwa kuwahusisha waandishi 30 waliopewa mafunzo na Mamlaka juu ya tatizo la dawa za kulevya Nchini na namna bora ya kuuhabarisha Umma ili kusaidia kuondokana na matumizi na biashara ya dawa za kulevya.

Alihitimisha kwa kusema, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya inatambua mchango wa wanahabari katika kufanikisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Hivyo, itaendelea kushirikiana nao ili sehemu kubwa ya jamii ifikiwe na elimu juu ya madhara yatokanayo na dawa za kulevya na hatimaye washiriki kwa pamoja katika mapambano hayo.



*WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akimkabidhi zawadi Veronica Romwald Mrema, mshindi wa kwanza wa shindano la kumpata mwandishi wa habari za kimtandao (digital journalist) aliyeandika habari za dawa za kulevya kwa umahiri.*



*WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akimkabidhi zawadi Abel Kilumbu, mshindi wa pili wa shindano la kumpata mwandishi wa habari za kimtandao (digital journalist) aliyeandika habari za dawa za kulevya kwa umahiri.*



*WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akimkabidhi zawadi John Laurent, mshindi wa tatu wa shindano la kumpata mwandishi wa habari za kimtandao (digital journalist) aliyeandika habari za dawa za kulevya kwa umahiri.*

Nanenane

# DCEA yaacha alama Nanenane 2022



*BAADHI ya wananchi wakitoa maoni kuhusu tatizo la dawa za kulevya walipotembelea banda la Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya katika Maadhimisho ya Nanenane Mbeya.*

**Na. MWANDISHI Wetu**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imeshiriki Maonesho ya Kitaifa ya Sikukuu ya wakulima Nanenane yaliyofanyika katika viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya kwa lengo la kutoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya.

Wananchi wa kada mbalimbali walitembelea banda la Mamlaka na kupata elimu juu ya dawa za kulevya. Vilevile, walipata fursa ya kuuliza maswali na kutoa maoni juu ya kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya.

*Inaendelea Ukurasa wa 19*

***KUPITIA banda la Mamlaka nimejifunza na kujua ukubwa wa tatizo la dawa za kulevya Nchini. Awali sikujua zipo dawa za kawaida za binadamu ambazo zikitumika vibaya zina madhara sawa za dawa za kulevya. Kama kiongozi nitatumia elimu hii kuwaelimisha wananchi wangu hususani vijana ambayo ndiyo kundi kubwa linaloathiriwa zaidi na dawa za kulevya."***



**Mhe. Sebastian Waryuba**
**Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga**



**Lilian Sambo**
**Mkurugenzi wa Lilian Greenport Co. LTD**

***HATUWEZI kutenganisha shughuli za kilimo na elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya. Mamlaka ishirikiane na wadau wa kilimo na kuyatumia madarasa ya kilimo kuelimisha Umma juu ya tatizo la dawa za kulevya. Njia hii itawasaidia wakulima kutojiingiza kwenye kilimo cha bangi na mirungi na badala yake walime mazao halali."***

Nanenane

# DCEA yaacha alama Nanenane 2022

*Inatoka Ukurasa wa 18*

*NIMEFAIDIKA na elimu inayotolewa na Mamlaka katika maonesho ya Nanenane, kwani nimefahamu aina mbalimbali za dawa za kulevya na madhara yake kiafya na kiuchumi. Nimejifunza kuwa, dawa za kulevya hazina umuhimu wowote ule zaidi ya kutuyumbisha vijana na kupoteza malengo yetu kimaisha. Nawaasa vijana wenzangu kutoshawishika kutumia wala kubeba dawa za kulevya kwani athari zake ni kubwa kwetu na Taifa kwa ujumla".*



**Zahra Masoud**
**Mwanafunzi wa Chuo cha Utabibu Uyole**

Pamoja na maoni hayo Kamishna Jenerali wa Mamlaka Gerald Kusaya akizungumza na waandishi wa habari katika kilele cha Maadhimisho ya Nanenane amesema Mamlaka imeshiriki Maonesho ya Nanenane Kitaifa mkoani Mbeya kuwaeleza watanzania hasa wakulima kwamba, dawa za kulevya zina athari na zinaharibu nguvu kazi ya Taifa.

Aliwakumbusha wakulima kuyatumia vyema mafunzo wanayoyapata kwenye maonesho ya nanenane kuzalisha mazao halali na kuachana na kilimo cha bangi na mirungi kwani ni kosa kisheria na adhabu yake inaweza kufikia hadi kifungo cha maisha.

*SISI kama Mamlaka inayoongoza mapambano dhidi ya dawa za kulevya Nchini, tunapiga vita dawa za kulevya kwa nguvu zote ili kila mtanzania popote alipo apate elimu kuhusu dawa hizi. Asitokee mtu amejiingiza kwenye matumizi na biashara ya dawa za kulevya kwa kukosa elimu na akifanya hivyo atakuwa amefanya kwa makusudi. Uwepo wetu hapa umesaidia wananchi kufahamu kuwa, dawa za kulevya zina athari kubwa Kiafya, Kijamii, Kiuchumi, Kimanzingira na Kisiasa". Amesema Kamishna Jenerali Kusaya.*






*KAMISHNA wa Kinga na Tiba wa Dkt. Peter Mfisi akifafanua jambo kwa Mkemia Mkuu wa Serikali Dkt. Fidelice Mafumiko alipotembelea banda la Mamlaka katika Maadhimisho ya Kitaifa ya Nanenane Mbeya.*




*WATUMISHI wa DCEA walipotembelea Nyumba ya Upataji Nafuu ya Women's Hope Rehab iliyopo Bagamoyo Pwani katika kuadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma.*

# Waraibu wanufaika na wiki ya utumishi wa Umma

**Na. MWANDISHI Wetu**

MAADHIMISHO ya Wiki ya Utumishi wa Umma hufanyika tarehe 16 hadi 23 mwezi Juni, kila mwaka. Maadhimisho haya hufanyika kwa lengo la kukumbushana wajibu na haki za watumishi wa Umma katika kuwaletea wananchi maendeleo hasa katika sekta ya kutoa huduma bora kwa wananchi. Maadhimisho haya huambatana na kauli mbiu mbalimbali ambapo kwa mwaka 2022 kauli mbiu ilikuwa ni ***"Uhusiano kati ya uwezeshaji wa vijana na usimamizi wa masuala ya uhamiaji: Kujenga utamaduni wa Utawala Bora, matumizi ya TEHAMA na ubunifu katika utoaji wa Huduma Jumuishi".***

Mwaka 2022, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ilishiriki

> Kwa kutambua umuhimu wa maadhimisho hayo, watumishi wa DCEA walitoa huduma mbalimbali katika kliniki ya Methadone Bagamoyo.

Maadhimisho haya kwa kufanya ziara katika Kliniki ya Methadone Bagamoyo, Nyumba ya Upataji Nafuu ya Women's Hope Rehab iliyopo Bagamoyo mkoani Pwani pamoja na Nyumba ya Upataji Nafuu ya Changamoto ni Matumaini iliyopo katika mkoa wa Dar es Salaam.


Wakati wa ziara hiyo, watumishi wa Mamlaka walitoa huduma katika kliniki ya Methadone Bagamoyo kwa kutoa dawa ya Methadone kwa waraibu wa dawa za kulevya waliofika kupata huduma pamoja na kutoa huduma za unasihi na msaada wa kisheria. Aidha, walifanya usafi kwenye jengo na maeneo yanayozunguka kituo hicho.

Katika nyumba za upataji nafuu za **Women's Hope Rehabilitation Center** iliyopo Bagamoyo inayohudumia waraibu wanawake na kituo cha **Changamoto ni Matumaini** kilichopo katika mkoa wa Dar es salaam inayohudumia waraibu wanaume. Mamlaka ilishiriki kutoa huduma za afya, unasihi, msaada wa kisheria na mahitaji mengine ya kibinadamu kwa waraibu wa dawa za kulevya.

# Sheria inasemaje kuhusu bangi



Kiasi cha bangi kisichozidi **gramu 50** na bangi iliyosindikwa isiyozidi **gramu Tano...**



...adhabu yake ni faini isiyopungua **shilingi milioni moja...**



...au kifungo cha **miaka mitano** jela.

**Na. MWANDISHI Wetu**

SHERIA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Namba 5 ya Mwaka 2015 inatafsiri mmea wa bangi kuwa ni mmea wowote wa bangi unaojumuisha sehemu yoyote ya mmea huo iliyo na kemikali ya haidrokanabino. Aidha, Sheria imetoa ufafanuzi kuhusu "bangi iliyosindikwa" kuwa ni utomvu usiochujwa au uliochujwa unaopatikana kutoka katika mmea wa bangi;

Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya inaharamisha kosa la kujihusisha na bangi kwa kutoa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka thelathini jela kwa mtu atakayetiwa hatiani akijihusisha na dawa hiyo ya kulevya kwa makosa yafuatayo: -

- **i.** Kulima bangi;
- **ii.** Kusambaza mbegu zinazozalisha bangi;
- **iii.** kumiliki, kuwa msimamizi au kuwa na mamlaka kwenye jengo, eneo au mahali, kuruhusu maeneo haya kutumika kwa ajili ya kilimo cha bangi;

Makosa mengine kuhusiana na bangi yanayoharamishwa na Sheria hii ni kuzalisha, kukutwa na bangi, kuuza, kununua, kusafirisha, kuingiza ndani ya Tanzania Bara, kusafirisha kwenda nje ya Tanzania Bara, kutumia au kufanya jambo lolote au kuzembea kufanya jambo linalohusiana na mimea ya bangi kitendo ambacho kipo kinyume na masharti ya Sheria hii.

## Mahakama kuhusiana na mashauri ya bangi

Kesi za bangi zinasikilizwa na Mahakama za chini au Mahakama Kuu kulingana na uzito wa kosa husika. Kifungu cha 2 kinafafanua kuwa makosa ya kujihusisha na bangi mfano kulima bangi au kusambaza mbegu zinazozalisha bangi au makosa mengine kama yalivyofafanuliwa chini **ya kifungu cha 11** cha Sheria, Mahakama yenye uwezo wa kusikiliza makosa hayo ni Mahakama za chini.

Aidha, **Kifungu cha 2** kinafafanua kuwa Mahakama za chini zina uwezo wa kusikiliza mashauri ya bangi yenye uzito usizidi kilo mia kuendana na matakwa ya **kifungu cha 15A.** Mashauri kuhusiana na kujihusisha na bangi zaidi ya kilo mia yanapaswa kusikilizwa na Mahakama Kuu.

## Matumizi ya bangi

Matumizi ya bangi ni kosa kisheria ambapo Vifungu vya 17 na 18 vinakataza matumizi ya dawa za kulevya ikiwemo bangi.

Kulingana na matakwa ya **kifungu cha 17**, kukutwa na kiasi kidogo cha bangi kwa matumizi binafsi ambacho kwa mujibu wa **Kanuni ya Tatu** ya Kanuni za Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, kiasi kidogo cha bangi ni kisichozidi **gramu 50** na bangi iliyosindikwa ni kiasi kisichozidi **gramu Tano** adhabu yake ni faini isiyopungua milioni moja au kifungo cha miaka mitano.

Aidha, Kazi ya kuithibitishia Mahakama kuwa kiwango alichokutwa nacho mtuhumiwa ni kwa ajili ya matumizi yake binafsi ni kazi ya mtuhumiwa.

Kifungu **cha 18** kinatoa adhabu ya faini isiyopungua milioni moja au kifungo cha miaka mitatu au adhabu zote kwa pamoja kwa mtuhumiwa atakayetiwa hatiani kwa makosa ya kujihusisha na matumizi ya bangi, kukutwa na vifaa vinavyohusiana na matumizi ya bangi au kukutwa kwenye nyumba, chumba, au eneo linalotumiwa kwa ajili ya matumizi ya bangi bila sababu yoyote ya msingi.

## Zuio la mmiliki au mtumiaji wa eneo

Sheria inakataza mtu ambaye ni mmiliki, mtumiaji, au mtu anayehusika na usimamizi wa eneo lolote, boma, chombo cha usafirishaji, kuruhusu vitumike kwa lengo la kulima, kutayarisha, kusafirisha, kuvuta au kuuza bangi au vinginevyo kutumia dawa hiyo kwa namna yoyote ile.

## Dhamana kwa makosa ya bangi

Kifungu **cha 29** cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kinahusika na dhamana kwa makosa yote ya dawa za kulevya. Kifungu hiki kinafafanua kuwa kwa makosa ya kujihusisha na bangi iliyosindikwa uzito wa kuanzia gramu 20 na kuendelea pamoja na makosa ya bangi kuanzia kilo 20 na kuendelea hayana dhamana.

## Katuni


CHEKI VIWALO VILE, PALE SIKOSI BUKU 5 YA FASTA
WE SEBENE!
KILA NIKIKWAMBIA UFUE NGUO ZAKO HUTAKI... NIMEKUFULIA UNAANUA MBICHI. UNAZIPELEKA WAPI?
HILI BANGI BALAA!

MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

**DCEA**

SCAN ME

**DIRA YETU:** Tanzania isiyojihusisha na biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

**DHIMA YETU:** Kudhibiti na kupambana na biashara na matumizi ya dawa za kulevya kupitia mikakati ya kisekta kwa ajili ya ustawi wa taifa.


Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana
na Dawa za Kulevya
S.L.P 80327
Dar es Salaam

8 Barabara ya Kivukoni,
11486 Dar es Salaam

**Simu:** +255 22 211 3754/57
**Nukushi:** +255 22 211 3752
**Barua pepe:** cg@dcea.go.tz
info@dcea.go.tz

***Namba ya Mawasiliano Bila Malipo (Call Centre) 119***

@dceatanzania
@dceatanzania
@dcea tanzania
DCEATV
www.dcea.go.tz